JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# MKUTANO WA TATU

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA SITA

**27 APRILI, 2016**

**MKUTANO WA TATU-YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU**

**TAREHE 27 APRILI, 2016**

## I. DUA

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Dkt Tulia Ackson (NAIBU SPIKA) alisoma Dua na kuliongoza Bunge.

**Makatibu Mezani**

1. Ndg. Nenelwa M. Wankanga
2. Ndg. Theonest Ruhilabake
3. Ndg. Zainab Issa
4. Ndg. Neema Msangi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

- Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) aliwasilisha mezani Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

- Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) Mhe. Angellah Jasmine Kairuki aliwasiisha mezani Hotuba ya Bajeti ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

- Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa Mhe. Jasson Rweikiza aliwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Vile vile aliwasilisha mezani maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

- Mhe. Mchungaji Peter Simon Msigwa, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora aliwasilisha Mezani Taarifa za Kambi kuhusu Wizara zote mbili kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## III. MASWALI

### 1. OFISI YA WAZIRI MKUU
Swali Na. 51: Mhe. Esther Michael Mmasi
Swali la nyongeza: Mhe. Esther Michael Mmasi

### 2. WIZARA YA NISHATI NA MADINI
Swali Na. 52: Mhe. Selemani Jumanne Zedi
Swali la nyongeza: Mhe.Selemani Jumanne Zedi

**3. WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Swali Na. 53: Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed
Swali la nyongeza: Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed

Swali Na. 54: Mhe. John Elias Kwandikwa
Swali la nyongeza: Mhe. Elias John Kwandikwa

**4. WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na. 55: Mhe Vedastus Mathayo Manyinyi [k.n.y Mhe. Lameck Okambo Airo]
Swali la nyongeza: Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi

Swali Na. 56: Mhe. Suzan Limbweni Kiwanga
Swali la nyongeza: Mhe. Suzan Limbweni Kiwanga

**5. WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Swali Na. 57: Mhe. Cecilia Daniel Paresso[ kny. Mhe.Joshua Nassari]
Swali la nyongeza: Mhe.Cecilia Daniel Paresso.

**6. WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Swali Na. 58: Mhe. Musa Rashid Ntimizi

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Musa Rashid Ntimizi
(ii) Mhe. Savelina Silvanus Mwijage

**7. WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

Swali Na. 59: Mhe. Masoud Abdallah Salim
Swali la nyongeza: Mhe. Masoud Abdallah Salim

Swali Na. 60: Mhe. Fatuma Hassan Toufiq

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Fatuma Hassan Toufiq
(ii) Mhe. Janet Zebedayo Mbene

**MATANGAZO**

1. Wageni mbalimbali walitambulishwa na Mhe. Naibu Spika.

2. Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitangaziwa kukutana saa 7:00 mchana Jengo la Utawala ukumbi Na. 227;

3. Kamati ya Miundombinu ilitangaziwa kukutana Saa 7:00 mchana, Jengo la Utawala ukumbi 229

Baada ya matangazo hayo Naibu Spika alitoa Mwongozo ulioombwa na Mhe. Hussein Mohamed Bashe tarehe 25 Aprili, 2016 kuhusu uhalali wa Upinzani kupewa posho na mishahara bila kuchangia Bungeni.

Pia alizungumzia na kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kutotumia Lugha za kuudhi wakati wote wanapochangia Mijadala au kuuliza Maswali na suala la staha kwa Wabunge.

**IV. MWONGOZO WA MHE. SPIKA**

1. Mhe. Kasuku Samson Bilago aliomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na 44(4) kwamba kwa nini ruhusa haikutolewa kuulizwa kwa Maswali ya nyongeza.

   Mhe. Naibu Spika alitoa maelezo kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaposoma Kanuni ya 44(4) wasome pamoja na Kanuni ya 43 inayozungumzia muda wa Maswali na mamlaka ya Spika.

2. Mhe. Ally Saleh Ally alieleza kutoridhishwa na majibu ya Waziri wa Katiba kuhusu suala la Mashekhe walioko ndani kwa miaka 3 bila ya kupelekwa Mahakamani.

   Mhe. Naibu Spika alisema litajibiwa baadaye.

3. Mhe. Esther Nicholaus Matiko aliomba mwongozo kufuatia mwongozo uliotolewa na Mhe. Naibu Spika kuhusu mwongozo wa Mhe. Hussein Bashe kwamba kwa nini wakati inasubiriwa kufanyika marekebisho ya Sheria na Kanuni usiwekwe utaratibu wa kulipa posho kwa kutumia Hansard.

   Mhe. Naibu Spika alieleza kwamba utatafutwa utaratibu wa namna ya kubadili Sheria na Kanuni zetu ili kulipa Wabunge posho zao hivyo maoni ya Mhe. Ester Nicholas Matiko yatachukuliwa wakati huo.

4. Mhe. Godbless Jonathan Lema alitumia Kanuni ya 149 kwanini wageni wetu wanaofika Bungeni wanarudishiwa getini wanapovaa min-skirt na wakati huo huo wageni (wa mataifa mengine ) wanaruhusiwa?

   Mhe. Naibu Spika alijibu kuwa Mpimaji wa vazi la heshima ni yule anayeruhusu mgeni kuingia au kutokuingia ndani ya Bunge.

**V. HOJA ZA SERIKALI**

Majadiliano yaliendelea kwa Mhe. Jenista Joakim Mhagama (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kuanza kujibu Hoja za Wabunge kwa dakika 30. Baada ya hapo Mhe. Waziri Mkuu alihitimisha Hoja yake kwa kutoa ufafanuzi wa Hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wabunge.

**VI. KAMATI YA MATUMIZI**

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi na kupitisha Mafungu yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake bila marekebisho.

Aidha, wakati wa Mshahara wa Waziri Mhe. Ruyagwa Zitto Kabwe aliomba mwongozo kuwa je siku hizi mshahara wa Waziri wachangiaji huteuliwa na vyama?

Naibu Spika alimjibu kwa kutumia Kanuni ya 101(3) na (4)

Baada ya Kamati ya Matumizi Bunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati, Bunge lilihojiwa na kupitisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**VII. KUSITISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Shughuli za Bunge zilisitishwa saa 6:30 mchana hadi saa 10:00 jioni.

**VIII. BUNGE KURUDIA**

Saa:10:00 jioni Bunge lilirejea na kuongozwa na mwenyekiti Mhe. Andrew John Chenge.

**IX. HOJA ZA SERIKALI**

1 Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) iliwasilishwa na Mhe. George Simbachawene kwamba Bunge likubali kupitisha madakirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

2 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) Mhe. Angellah Jasmine Kairuki aliwasilisha Hoja yake kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

3 Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa aliwasiisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) kwa

Mwaka wa Fedha 2015/2016 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya TAMISEMI na Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

4 Mhe. Japhary Raphael Michael Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI aliwasilisha Maoni ya Kambi hiyo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

5 Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani – Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) aliwasilisha Maoni ya Kambi hiyo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Kabla ya Wabunge kuanza kuchangia Hoja ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) Mhe. Andrew John Chenge aliwasilisha Waraka wa Spika Na. 04/2016 wa Mabadiliko ya Wajumbe wa Kamati za kudumu za Bunge.

**MWONGOZO WA SPIKA**

Mhe. Cecilia Daniel Paresso alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kwamba wakati Mhe. Waziri Mku anahitimisha Hoja yake alikiri kuwepo upungufu wa Sukari na kwamba Serikali imeshaagiza sukari nje ya nchi wakati hapo nyuma Serikali ilisema haitaagiza sukari toka Nje ya Nchi. Sasa mbona inakuwa kigeugeu. Mwenyekiti kaagiza Serikali isambaze statement ya Waziri wa Fedha wakati anachangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mwenyekiti alijibu kuwa Mhe. Spika ndio mwenye mamlaka ya kusema jambo hili linaruhusiwa au la.

Waheshimiwa wafuatao walipata nafasi ya kuchangia Hoja ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utuishi na Utawala Bora):-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Esther Lukago Midimu | - | CCM |
| 2. | Mhe. Felister Aloyce Bura | - | CCM |
| 3. | Mhe. Mendrad Lutengano Kigola | - | CCM |

## X. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE

Saa 2:00 Usiku Mwenyekiti aliahirisha Bunge hadi tarehe 28/4/2016 saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**27 APRILI, 2015** **KATIBU WA BUNGE**